

HUKUMU ZA FUNGA.

Hukumu ya swaumu:

Swaumu ya mwezi wa Ramadhan ni nguzo katika nguzo za uislamu tano, kwa kauli yake Mtume (saw):

(Uislamu uwejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudilia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, kusimamisha swala tano, kutoa zakat, kuhiji na kufunga mwezi wa Ramadhan.) (ameipokea Bukhar na Muslim:8, 16).

Maana ya swaumu, swaumu ni kujizuia na kula, kunywa, kufanya tendo la ndoa, na vyote vyenye kufunguza kuanzia kuchomoza kwa alfajir mpaka kuzama kwa jua kwa nia ya kujikurubisha kwa Allah (sw).

Swaumu ya Ramadhani ni wajibu Allah anasema:

(Yeyote mwenye kuushudia mwezi hali ya kuwa sio mgonjwa wala msafiri basi aufunge mwezi huo) (Al-Baqara: 185).

Kufunga ni wajibu kwa kila muislamu aliefikia baleghe mwenye akili timamu, na baleghe inapatikana pale kijana anapofikia miaka kumi na tano na kuota nywele za sehemu za siri, au kutokwa na manii kwa kuota au kwa namna nyingine, na inazidi kwa mwanamke kwa kutokwa na hedhi, anapopata mtu moja ya vitu hivi basi amebaleghe.

UBORA WA MWEZI WA RAMADHAN.

Mwenyezi Mungu ameuteua mwezi wa Ramadhan kuwa ni mwezi wenye fadhila nyingi kulikoni miezi mingine kutokana na nyakati zake, miongoni mwa fadhila zake;

1. Kwamba malaika wanawaombea wenye kufunga msamaha mpaka wafungue.
2. Wanafungwa mashetani waovu.
3. Ndani ya mwezi Ramadhani kuna usiku wa Laylatul Qadir ambao ni bora kuliko miezi elfu moja.
4. Wanapata msamaha wenye kufunga kila mwisho wa usiku wa Ramadhan.
5. Allah anawaachia huru na moto kila usiku wa Ramadhan.
6. Kwamba kufanya umrah ndani ya mwezi wa Ramadhan ni sawa na kufanya Hija.

Na mionganoni mwa yale yaliyopokewa kutokana na ubora wa mwezi wa Ramadhan ni Hadithi aliyopokea Abu Huraira (R.A) anasema, Amesema Mtume (saw):

(Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa ana Imaani na kutarajia thawabu, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 38, 760).

Mtume (saw) anasema kuhusu swaumu:

(Kila matendo afanyayo mwanadamu yatazidishwa mara difu, jema moja kwa thawabu kumi mpaka mia saba, Mwenyezi Mungu anasema: Isipokuwa swaumu, kwani hakika ya swaumu ni yangu na mimi ndie nitakaeilipa) (Ameipokea Bukhar na Muslim:5927, 1151).